# PHILOBUS, KASISI WA KOPTIKI WA MISRI NA MMISIONARI (SEHEMU YA 1 KWA 2)

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Kasisi ambaye wakati mmoja alieneza kwa bidii imani potofu kuhusu Uislamu anaukubali Uislamu (sehemu ya 1).

**Aina:** Makala Hadithi za Waislamu Wageni Makasisi na Wakilishi wa Kidini

**Na:** Ibrahim Khalil Philobus

**Iliyochapishwa mnamo:** 17 Dec 2021

**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021

Al-Haj Ibrahim Khalil Ahmad, zamani alijulikana kama Ibrahim Khalil Philobus, alikuwa kasisi wa Koptiki wa Misri aliyesomea theolojia na kupata shahada ya juu kutoka Chuo Kikuu cha Princeton. Aliusoma Uislamu ili kupata mapengo ya kuushambulia; badala yake alisilimu pamoja na watoto wake wanne, mmoja wao ambaye sasa ni profesa mahiri katika Chuo Kikuu cha Sorbonne, Paris Ufaransa. Kwa njia ya kuvutia, anajidhihirisha akisema:

“Nilizaliwa Alexandria tarehe 13 Januari 1919 na nilipelekwa katika shule za Misheni za Marekani hadi nilipopata cheti cha elimu ya sekondari huko. Mnamo 1942 nilipata diploma yangu kutoka Chuo Kikuu cha Asiut na kisha kubobea katika masomo ya kidini kama utangulizi wa kujiunga na Kitivo cha Theolojia. Haikuwa kazi rahisi kujiunga na kitivo, kwani hakuna mtahiniwa aliyeweza kujiunga hadi apate pendekezo maalum kutoka kwa kanisa, na pia baada ya kufaulu mitihani kadhaa migumu. Nilipata pendekezo kutoka kwa Kanisa la Al-Attareen huko Alexandria na lingine kutoka Church Assembly of Lower Egypt baada ya kufaulu majaribio mengi ya kujua sifa zangu za kuwa mtu wa dini. Kisha nikapata pendekezo la tatu kutoka Snodus Church Assembly ambalo lilijumuisha makasisi kutoka Sudan na Misri.

Snodus iliidhinisha kuingia kwangu katika Kitivo cha Theolojia mnamo 1944 kama mwanafunzi wa bweni. Huko nilisoma na walimu Wakimarekani na Wamisri hadi nilipohitimu mwaka wa 1948.

Nilipaswa, na kuendelea , kuteuliwa ndani ya Yerusalemu, kama si kwa ajili ya vita vilivyoanza Palestina mwaka huo huo, nilitumwa Asna katika Misri ya Juu. Mwaka huo huo nilijiandikisha kwenye tasnifu katika Chuo Kikuu cha Marekani huko Cairo. Ilihusu shughuli za kimisionari kati ya Waislamu. Ujuzi wangu na Uislamu ulianzia katika Kitivo cha Theolojia ambapo niliusoma Uislamu na mbinu zote ambazo kupitia hizo tunaweza kutikisa imani ya Waislamu na kuibua imani potofu katika ufahamu wao wa dini yao wenyewe.

Mnamo mwaka wa 1952 nilipata M.A. kutoka Chuo Kikuu cha Princeton huko Marekani na nikateuliwa kuwa mwalimu katika Kitivo cha Theolojia huko Asiut. Nilikuwa nikiufundisha Uislamu katika kitivo pamoja na imani potofu zilizoenezwa na maadui zake na wamishenari dhidi yake. Katika kipindi hicho, niliamua kupanua masomo yangu ya Uislamu ili nisisome vitabu vya wamishenari juu yake tu. Nilikuwa na imani sana ndani yangu hadi kutaka kusoma maoni mengine. Hivyo nilianza kusoma vitabu vilivyoandikwa na waandishi wa Kiislamu. Pia niliamua kusoma Quran na kuelewa maana yake. Hili lilidokezwa na kupenda kwangu elimu na kusukumwa na hamu yangu ya kuongeza uthibitisho zaidi dhidi ya Uislamu. Matokeo yalikuwa, hata hivyo, kinyume kabisa. Msimamo wangu ulianza kutetereka na nikaanza kuhisi mapambano makali ya ndani, na nikagundua uwongo wa kila kitu nilichokuwa nimesoma na kuwahubiria watu. Lakini sikuweza kujikabili kwa ujasiri na kujaribu badala yake kushinda shida hii ya ndani na kuendelea na kazi yangu.

Mnamo mwaka 1954, Bw. Khalil aliongeza, nilitumwa Aswan kama katibu mkuu wa Misheni ya Uswizi ya Ujerumani. Hiyo ndiyo ilikuwa kazi yangu, ila dhamira yangu halisi ilikuwa ni kuhubiri uovu dhidi ya Uislamu huko Misri ya Juu hasa miongoni mwa Waislamu. Kongamano la wamishonari lilifanywa wakati huo katika Hoteli ya Cataract huko Aswan, nami nikapewa nafasi ya kuzungumza. Siku hiyo nilizungumza sana, nikirudia imani potofu zote zinazorudiwa dhidi ya Uislamu; na mwisho wa hotuba yangu, mgogoro wa ndani ulinijia tena na nikaanza kurekebisha msimamo wangu.

Akiendelea na mazungumzo yake kuhusu mgogoro huo, Bw. Khalil alisema, “Nilianza kujiuliza: Kwa nini niseme na kufanya mambo yote haya ninayojua kwa hakika mimi ni mwongo, kwani huu si ukweli? Niliondoka kabla ya mwisho wa mkutano na nikatoka peke yangu kwenda nyumbani kwangu. Nilitetemeka. Nilipokuwa nikitembea kwenye bustani ya umma ya Firyal, nilisikia aya ya Quran kwenye redio. Ilisema:

***“Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur'ani ya ajabu! Inaongoza kwenye uwongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi.” (Kurani 72:1-2)***

***“Nasi tulipo usikia uwongofu tuliuamini. Basi mwenye kumuamini Mola wake Mlezi haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa.” (Kurani 72:13)***

Nilihisi faraja kubwa usiku huo, na niliporudi nyumbani nilikaa usiku mzima peke yangu katika maktaba yangu nikisoma Quran. Mke wangu aliniuliza kuhusu sababu ya kukaa kwangu usiku kucha na nikamsihi aniache peke yangu. Nilisimama kwa muda mrefu nikifikiria na kutafakari aya hii:

***“Lau kuwa tumeiteremsha hii Kurani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeli uona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu...” (Kurani 59:21)***

Na aya:

***“Hakika utawakuta walio shadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walio amini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanao sema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi. Na wasipo sikia yaliyo teremshwa kwa Mtume utaona macho yao yanachururika machozi kwa sababu ya Haki waliyo itambua. Wanasema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini. Basi tuandike pamoja na wanao shuhudia. Na kwa nini tusimuamini Mwenyezi Mungu na Haki iliyo tujia, na hali tunatumai Mola wetu Mlezi atuingize pamoja na watu wema?’” (Kurani 5:82-84)***

Kisha Bwana Khalil akanukuu nukuu ya tatu kutoka katika Quran Tukufu isemayo:

***“Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mungu ila Yeye anaye huisha na anaye fisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.” (Kurani 7:157-158)***

Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://www.islamreligion.com/index.php/sw/articles/105/philobus-kasisi-wa-koptiki-wa-misri-na-mmisionari-sehemu-ya-1-kwa-2

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2023 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.